

## SALA YA MAJITOLEO YA ASUBUHI (*Kwa wavaao skapulari*)

(*Kwa Ibada ya Skapulari ya Brouwn ya Mlima Karmeli.*)

Mungu wangu, nikiungana na Moyo safi wa Maria (hapo busu Skapulari yako kama alama ya majitoleo yako) nakutolea damu takatifu ya thamani sana ya Yesu inayotolewa leo altareni duniani kote, nikiunganisha nayo kila wazo, neon na tendo la siku hii ya leo.

Ee Yesu, nataka leo hii kupata kila rehema na mastahili niwezayo kupata na nazitolea pamoja na nafsi yangu kwa Moyo safi wa Maria, ili Yeye avitolee kwa yale yanayohitajiwa kwa kutuliza Moyo wako Mtakatifu.

Damu Takatifu ya Yesu,

Utuokoe!

Moyo Safi wa Maria

Utuombee!

Moyo Mtakatifu wa Yesu,

Utuhurumie!